



25/09/2024

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KIBAHA, ANATANGAZA UWEPO WA FEDHA KWAAJILI YA KUVIKOPESHA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU AMBAPO JUMLA YA SHILINGI 1,169,428,549.05. (*Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Sitini na tisa, Laki Nne Ishirini na Nane, Mia Tano Arobaini na Tisa na Senti Tano Tu*) ZIMETENGWA KATIKA ROBO YA PILI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. HIVYO VIKUNDI VYENYE SIFA VINAKARIBISHWA KULETA MAOMBI KATIKA OFISI YA AFISA MTENDAJI WA KATA ZILIZOPO KWENYE MAENEO YENU.

VIKUNDI VINAVYOTAKIWA KUOMBA MIKOPO VINAPASWA KUWA NA SIFA ZIFUATAZO:

- (i) KIKUNDI CHA WANAWAKE,VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KILICHOTAMBULIWA NA KUPEWA CHETI CHA UTAMBUZI NA HALMASHAURI,
- (ii) KIKUNDI KIWE KINAJISHUGHULISHA NA SHUGHULI ZA UJASIRIAMALI MDOGO AU WA KATI AU KIKUNDI KINACHOTARAJIA KUANZISHA SHUGHULI ZA UJASIRIAMALI,
- (iii) KIKUNDI CHA WANAWAKE NA VIJANA KIWE NA IDADI YA WANAKIKUNDI KUANZIA WATANO(5) NA KUENDELEA NA KIKUNDI CHA WATU WENYE ULEMAVU KIWE NA WANAKIKUNDI WASIOPUNGUA WAWILI(2). PIA MTU MWENYE ULEMAVU ANAWEZA KUWA NA SIFA YA KUPATA MKOPO KAMA KIKUNDI CHA WATU WENYE ULEMAVU ENDAPO TIMU YA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI ITAJIRIDHISHA KUWA AMEKOSA MTU Mwingine MWENYE ULEMAVU WA KUUNGANA NAYE KATIKA ENEO LAKE,
- (iv) KIKUNDI KIWE NA AKAUNTI YA BENKI ILIYOFUNGULIWA KWA JINA LA KIKUNDI KWAAJILI YA SHUGHULI ZA KIUJASIRIAMALI; NA
- (v) WANA KIKUNDI LAZIMA WAWE NI RAJA WA TANZANIA WASIO NA AJIRA RASMI, WENYE AKILI TIMAMU NA WENYE UMRI WA KUANZIA MIAKA 18 NA KUENDELEA. AIDHA, KIKUNDI CHA VIJANA KITAPASWA KUWA NA WANAKIKUNDI WENYE UMRI KUANZIA MIAKA 18 HADI 45.

S. L. P 30112,KIBAHA PWANI, Simu +255 232402938, Nukushi + 255 232402007
1 Mtaa wa Halmashauri 61182 Kibaha CBD, Barua pepe: td@kibahatc.go.tz, Tovuti www.kibahatc.go.tz.

MAOMBI YOTE YATUMWE KUPITIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (*WEZESHA PORTAL*) ILI KUTAMBULIWA NA KUOMBA MKOPO AU WASILIANA NA AFISA MAENDELEO YA JAMII WA KATA HUSIKA AU MTENDAJI WA KATA HUSIKA.

KIKUNDI KINACHOOMBA MKOPO KINAPASWA KUWA NA VIAMBATANISHO VIFUATAVYO:

- (i) BARUA YA KIKUNDI YA KUOMBA MKOPO ILIYOPITISHWA NA AFISA MTENDAJI WA MTA A NA KATA,
- (ii) MUHTASARI WA KIKUNDI WA KUOMBA MKOPO ,
- (iii) ANDIKO RAHISI LA MRADI UNAOOMBEWA MKOPO,
- (iv) KATIBA YA KIKUNDI ILIYO NA MAJINA YA WANAKIKUNDI NA KUPITISHWA NA MWANASHERIA.
- (v) WAOMBAJI LAZIMA WAAMBATANISHE NAMBA/KITAMBULISHO CHA TAIFA(NIDA)

DIRISHA LA KUPOKEA MAOMBI YA MIKOPO KWA ROBO YA PILI KWA MWAKA 2024/2025 LITAKUWA WAZI KUANZIA TAREHE 5/10/2024 HADI 22/10/2024

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:

Dkt. ROGERS JACOB. SHEMWELEKWA
MKURUGENZI WA MJI
KIBAHA

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA